# Ubainishaji wa Viashiria vya Kiujumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya Teule za Kimajaribio

*Festo Joster* na *Elizabeth Mahenge*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala haya yanabainisha viashiria vya kiujumi katika riwaya ya Kiswahili yakijiegemeza katika riwaya teule za kimajaribio. Msukumo wa kushughulikia viashiria vya kiujumi katika riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio unatokana na kuwapo kwa madai kuwa riwaya za mkondo huu kama vile *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Kezilahabi hazina maana katika jamii ya Afrika Mashariki (Mbatia, 1998). Hii ina maana kuwa riwaya za mkondo huu hazina ujumi wowote katika kuleta maendeleo kwa jamii ya Afrika Mashariki. Riwaya kuwa na maana huanzia katika sababu za kuandikwa kwake Jones (1994). Kutokana na mpishano huo wa mawazo, tuliona ipo haja ya kuchunguza ujumi wa riwaya hizi za kimajaribio ili kubainisha viashiria vya kiujumi katika riwaya za Kiswahili. Ili kufikia matokeo ya utafiti huu riwaya teule mbili yaani *Bina-Adamu!* (2002) ya Wamitila na *Dunia Yao* (2006) ya Mohamed zilihakikiwa. Data kutoka uwandani zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji, mijadala ya vikundi na usaili. Data zilitoka kwa watoa taarifa wasomaji ambao ni wanafunzi wa Shahada ya Awali na Umahiri katika Kiswahili kutoka Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile wandishi wa riwaya husika kutoka Nairobi Kenya na Wete Pemba walihusika kutupatia data. Makala yaliongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi. Kwa kutumia mkabala wa kitaamuli tulichambua, tulichakata na kuwasilisha data. Matokeo yanaonesha kwamba riwaya za Kiswahili za kimajaribio zina viashiria vya kiujumi ambavyo vinadhihirisha ujumi wa riwaya hizi. Ujumi huo una mchango mkubwa sana katika firka za wasomaji kwa maendeleo ya Afrika Mashariki. Aidha, makala haya yanatia chachu kwa tafiti nyingine kuchunguza mbinu zinazowasaidia waandishi na wahariri kuukamilisha ujumi wa riwaya hizi.**

**Maneno Muhimu:** Ujumi, Vijenzi vya Kiujumi, Viashiria vya Kiujumi, Mwitiko

## Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Kumekuwapo na mgongano mkubwa wa kimawazo kuhusu umuhimu wa riwaya zinazojulikana kama riwaya za kimajaribio. Wengine huziona ni ngumu, tata na hazieleweki kutokana na sifa kadhaa zinazojitokeza katika riwaya hizo (Gromov, 2004, 2019 na Khamis, 2007a na b). Kutokana na ugumu huo kuna baadhi ya wataalamu wanaona hazina maana katika jamii (Mbatiah, 1998). Dai la Mbatiah lina maana kuwa riwaya hizi hazina ujumi wowote wa kimaendeleo katika jamii. Jambo linaloshangaza ni kuongezeka kwa utunzi wa riwaya za Kiswahili za mkondo huu kutoka mwaka 1990 hadi sasa Gromov (2014 na 2019). Jambo linalotia msukumo wa kuchunguza ujumi wa riwaya za kimajaribio katika jamii ya Afrika Mashariki.

## Dhana ya Ujumi

Barrett (2012) anaeleza kuwa ujumi una mizizi kutoka katika utamaduni wa falsafa ulioanzishwa katika karne ya 18. Utamaduni huo ulijikita katika msingi wa Wagiriki wa Kale ukijaribu kuelezea asili, maana na thamani ya sanaa na uzoefu wa kihisia katika kuwako kwa maisha ya mwanadamu. Ujumi ni dhana inayotokana na neno la Kiingereza *aesthetics* lenye asili ya Kigiriki *aisthetikos* likimaanisha hisi au utambuzi (Armstrong, 1879; Gallie, 1964; Barrett, 2002). Miaka ya 1735, Alexander Baumgarten aliitumia dhana hiyo kutoka katika lugha ya Kigiriki kwenda katika lugha ya Kijerumani kama *Ästhetisch* akiwa na maana ya "uhakiki wa ladha" (Barret, 2012, Lopes, 2015). Hadi kufikia katikati ya karne ya 18, dhana hiyo ilikuwa ikitumika katika falsafa kama sayansi

inayoshughulikia udhibiti wa utambuzi kwa hisi (Lopes, 2015). Kant 1790 aliweza kulitafsiri neno hilo katika lugha ya Kiingereza kama *aesthetic* na sasa linatumika katika maandiko mengi

Hadi kufikia katikati ya karne ya 20 tafiti kuhusu ujumi zimepanuka na kutumika katika nyanja mbalimbali kama vile falsafa, saikolojia, sosholojia na sanaa (Barret, 2012). Miongoni mwa nyanja hizo ujumi umefasiliwa kwa namna mbalimbali, na kila nyanja ina wananadharia wa ujumi wake wenyewe (Lankford, 1992). Katika uwanja wa sanaa na fasihi ikiwamo, ujumi huweza kufasiliwa kama sayansi ya uzuri wa kazi ya sanaa. Ujumi wa kisanaa katika fasihi, huonesha uzuri, mvuto na utamu wa kazi ya sanaa. Mvuto huo unapaswa kuonekana, kusikika na kuhisika (Kivy 2011; na Mulokozi 2017). Tunaweza kubaini ujumi huo kwa kusoma maneno yaliyomo katika vitabu na kupata mawazo yanayoathiri fikra za msomaji (Locke 1975; Kivy 2011).

Mulokozi (2017) anadai kuwa, dhima ya ujumi wa kifasihi huwa ni ile hali inayotokana na mvuto, mchomo na uzuri wake kisanaa na athari ya mambo hayo kwa hadhira. Dhima ya kiujumi inaweza kuwa chanya au hasi. Kwa upande wa uchanya huweza kuburudisha, kufurahisha, kuliwaza, kusisimua na kuelekeza (kuwa mfano wa kuigwa na watunzi wengine). Mawazo ya Mulokozi (2017) yanaelekea kuungana na mawazo ya Armstrong (1879) kuhusu uzuri wa kisanaa akidai kuwa, mvuto unaotokana na uzuri wa kisanaa hutokana na matumizi ya vijenzi vya kiujumi kwa kueleza mambo kwa hisia za ndani, matumaini, woga, furaha au huzuni, upendo au chuki na kadhalika. Vilevile hueleza mchomo wa moyo ambao hutikiswa ndani ya mwanadamu. Kwa upande wa uhasi dhima ya kiujumi kwa mujibu wa Mulokozi (2017) ni pamoja na kuudhi, kukera, kusikitisha na hata kupotosha kimwonekano au kihisia (uk. 24).

Kwa maelezo hayo, dhana ya ujumi inaweza kufasiliwa kuwa ni uzuri unaopatikana katika kazi ya fasihi ambao humvutia na kuathiri hisia za msomaji kutokana na matumizi ya vijenzi vya kiujumi[1]. Ujumi huweza kumvutia msomaji na kumwathiri kihisia kiasi cha kubadili, kuboresha au kuacha baadhi ya tabia alizonazo kutokana na uzoefu wa kiujumi alionao. Mabadiliko hayo huja kutokana na kuisoma kazi fulani ya fasihi. Hivyo kazi ya fasihi inaweza kuwa imefanikiwa kubeba dhima ya kiujumi endapo msomaji atavutiwa na kuathiriwa na kazi hiyo ya fasihi.

**Ujumi katika Kazi za Fasihi**

Kwa muda mrefu tangu enzi za Aristotle tafiti mbalimbali zilizojadili kuhusu ujumi zinathibitisha kuwapo kwa ujumi katika utanzu wa ushairi na tamthilia lakini ujumi katika utanzu wa riwaya haujaelezwa bayana (Rosenblatt, 1933; Ferrari, Kivy, 2011 na kadhalika). Kwa mfano Kivy (2011) anaamini kuwa kazi bunilizi na riwaya ikiwamo ni kazi zisizo na ujumi. Anaendelea kueleza kuwa, hata katika usomaji wa riwaya nia kuu ya msomaji ni kujiegemeza katika maudhui ya hadithi halafu masuala mengine hufuata. Masuala yanayotajwa na mtaalamu huyu ni kama vile wahusika, mandhari, usimulizi miongoni mwa mambo mengine. Ijapokuwa Kivy hatwambii zaidi kuhusu namna msomaji anavyovutiwa ili kuendelea kusoma riwaya hiyo na pengine mambo yanayoathiri mwelekeo wa uzoefu wa kiujumi aliyonao msoamji, bado kazi hii inatupa kujiuliza zaidi kuhusu mvuto huo unatokana na nini?

Puolakka (2019) anasogea mbele kidogo mawazo ya Kivy (2011) kwa kukiri kuwa riwaya ina ujumi kamili unaotoshelezwa na ukamilifu wa nyakati. Hii ina maana kuwa ule muunganiko mgumu na wakati mwingine muunganiko tata wa matukio katika riwaya huwa na maana kamili kinyakati. Puolakka anaeleza kuwa ni wazi kwamba riwaya ni utanzu mgumu kwa kuwa unahusisha vipengele mbalimbali tenganifu lakini kwa muunganiko wenye uchangamano kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano kuwa na wahusika wengi wenye namna tofautitofauti ya mahusiano baina ya mmoja na mwingine, hawa wote kwa umoja wao hukamilisha hadithi ya riwaya. Ili kukamilisha hadithi hiyo mwandishi huwapa tabia zinazokamilisha visa mbalimbali kwa uchangamano mkubwa. Wahusika wa riwaya huwa na sifa za kuvutia kisaikolojia na kiuhalisia. Wahusika hawa huingizwa katika msigano mkubwa

[1] Vijenzi vya kiujumi ni sifa au vipengele vya kifasihi vinavyobeba maudhui ya kazi ya fasihi (Henry, 2020, Walton 2004; Mtrevors na Levinson 2005; na Attard 2018).

wa muundo wa usimulizi wa mwandishi. Mpangilio wa visa, matukio, muundo na usimulizi unaobebwa na wahusika huufanya ujumi wa riwaya kuwa kamilifu kinyakati. Andiko la mtaalamu huyu linadokeza juu ya kuwapo kwa ujumi katika riwaya kwa kuhusisha uhusika na usimulizi katika kukamilisha hadithi katika riwaya. Ijapokuwa haliweki wazi suala la viashiria vya kijumi vinavyomvutia msomaji kiasi cha kumwathiri msomaji lakini andiko hili linadokeza kuwapo kwa ujumi katika riwaya.

Pickens (2014) alichunguza uandishi wa Octavia Butler na ujumi wa riwaya zake anaona kuwa mwandishi huyu ana utajiri wa kimaudhui juu ya mambo matatu ambayo ni rangi, jinsia na ulemavu na uhusiano wa mambo hayo na uwanawake wa mtu mweusi. Tukiungana na mawazo ya Pickens tunaona kwamba msomaji yeyote anapokutana na kazi ya Butler lazima au atarajie kukutana na maudhsui yanayohusu rangi, jinsia na ulemavu kwa kumhusianisha na mwanamke mweusi wa Kiafrika. Hali hii ina maana kuwa tunaweza kuupambanua ujumi wa mwandishi fulani wa kazi za fasihi kupitia kazi zake. Andiko hili linaonesha kuwa mwandishi anaweza kuwa na ujumi wake unaoweza kupambanuliwa kupitia kazi zake, lakini hajaweka wazi viashiria vya kiujumi vinavyojitokeza katika riwaya, hivyo kutoa mwanya kufanyika kwa tafiti nyingine.

Jones (1994) anajipambanua kama msomaji wa riwaya za dunia ya tatu (za kimajaribio) mbali na riwaya nyinginezo (za kiuhalisia). Jones anajipambanua kuwa ana mtazamo tofauti wa kiujumi kwa kuwa anapenda kazi zenye mafumbo mazito, ngumu au tata katika kuzifasili, riwaya zenye kejeli na sitiari nzito; kazi hizi ni sehemu ya utamaduni wake. Wakati mwingine hupenda kuunga mkono au kutatiza mantiki kulingana na hadhi ya mtu husika na pengine huunda mikanganyiko kwa maksudi. Maelezo haya yanaonesha sifa ya msomaji mwenye tajriba ya kupenda kazi za fasihi zenye sifa zinazokaribiana na riwaya za kimajaribio. Andiko hili linaonesha athari ya kazi za kifasihi ambazo humwathiri msomaji kwa kujenga tabia ambazo hakuwa nazo mwanzo lakini kutokana na kusoma kazi zilizojaa mafumbo, utata na ugumu hujikuta kuwa na tabia zinazofanana na sifa za riwaya hizo. Pamoja na kwamba maelezo haya yanaashiria kuathirika kwa msomaji kutokana na kazi hizo bado andiko hili haliweki wazi ikiwa sifa hizo ndiyo viashiria vya kiujumi, hivyo ipo haja ya kufanyika kwa uchunguzi zaidi ili kujiba pengo hilo.

Yakijumuishwa maelezo ya wataalamu hapo juu, tunaona kwamba kuna pengo la kiutafiti ambalo kimsingi linahitaji kuzibwa. Tafiti hizo haziweki wazi viashiria vya kiujumi vinavyozifanya riwaya zivutie, zinazomuathiri msomaji kiasi cha kuwa na tabia zinazoendana na sifa za riwaya husika na kadhalika. Makala haya yanashughulikia pengo hilo kwa kubainisha viashiria vya kiujumi katika riwaya.

Mjadala wa hapo juu umeeleza ujumi katika riwaya kiujumla. Ama kuhusu ujumi wa riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio mbali na mtazamo wa Mbatiah (1998) kuona kuwa riwaya za mkondo wa kimajaribio hazina maana au umuhimu wowote katika jamii, akitolea mifano kutoka katika riwaya ya *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Kezilahabi tunaona yanakanganya mno. Mbatia anadai kwamba riwaya hizo hazina maana katika jamii ya Afrika Mashariki kwa kuwa zinayaona maisha hayana maana. Anaendelea kueleza kuwa uandishi wa aina hii unarudisha nyuma sanaa ya uandishi badala ya kuupeleka mbele. Madai haya yanaonesha namna riwaya za mkondo wa kimajaribio zisivyokuwa na umuhimu katika jamii kwa kuwa haziburudishi wala kueleza matatizo ya jamii kwa uwazi, badala yake zinampa msomaji ugumu wa kuelewa ujumi uliyomo katika riwaya hizo. Kutokana na andiko hili, makala haya yanaona kuwa ijapokuwa Mbatia hakueleza kwa wazi kuhusu ujumi lakini mawazo yake yanaashiria kuwa riwaya za mkondo wa kimajaribio hazina ujumi, hivyo makala haya yanachunguza viashiria vya kiujumi katika riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio.

Pengine Mbatiah anasahau kuwa, mbali na riwaya za hadi miaka 1989 kumekuwapo na mabadiliko makubwa katika riwaya ya Kiswahili kifani na kimaudhui. Riwaya hizi zimefanikiwa kuichunguza jamii tena kwa kutumia mbinu mpya kabisa kuelezea matatizo ambayo si ya jamii ya Afrika Mashariki tu bali dunia nzima, (Gromov, 2004, 2016 na 2019). Mbinu hizo mpya ni zile zinazopatikana katika riwaya za kimajaribio kama vile *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Kezilahabi, *Zirairli na Zirani* (1999) ya Mkufya, *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za

Mohamed, *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2006) za Wamitila, *Mafamba* (2008), *Watu wa Gehenna* (2012) na *Mashetani ya Alepo* (2015) za Tom Olali na kadhalika (Gromov, 2019).

Lindi (2012) anaonesha wazi namna riwaya za kimajaribio zinavyochangia maendeleo katika jamii pana ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla. Anaeleza kuwa riwaya hizi zinasaidia kusukuma mbele maendeleo ya jamii ya Waswahili na kukuza kiwango cha uandishi. Ijapokuwa Hata hivyo Lindi hajabainisha viashiria vya kiujumi vinavyoonesha ujumi wa riwaya hizi bali amejadili tu mchango wa riwaya wake katika maendeleo ya jamii ya Afrika Mashariki. Kutokana na andiko la Lindi, tunaona kuwa riwaya za kimajaribio zina sababu za kuandikwa kwake kama Jones (1994) anavyoeleza kuwa, riwaya ina mahali pake pa kuanzia (chanzo chake), haiibuki tu bila sababu zozote zinazomsukuma mwandishi kuandika kwa ajili ya jamii yake. Kwa kuwa Lindi amechunguza suala la dhima za riwaya hizi na kuacha kubainisha viashiria vya kiujumi vinavyojitokeza katika riwaya hizi, tuliona ipo haja ya kufanyika uchunguzi zaidi ili kuziba pengo hili. Kutokana na hali hii makala haya yamebainisha viashiria vya kiujumi katika riwaya teule ya Kiswahili ya kimajaribio.

Fasihi andishi ina tanzu kuu tatu ambazo ni ushairi, nathari (hasa hadithi fupi na riwaya) na tamthilia (Mulokozi, 2017). Mbali na tanzu nyingine, utanzu wa nathari hasa riwaya una sifa ya kuwa na visa vingi vinavyoruhusu kutamba na kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Pia, riwaya ina wahusika wengi, mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani upana wa maisha ya jamii (Senkoro, 1982). Urefu na upana wa mawanda katika riwaya unautofautisha na tanzu nyingine kwa kuwa tanzu hizo zina ufinyu au ubanifu wa mawanda (Wamitila, 2008). Akizungumzia sifa ya urefu na upana, Madumulla (2009) anadai kuwa inaupa uwezo utanzu huu kumeza tanzu nyingine za fasihi andishi katika mawanda yake. Kutokana na sababu hiyo tulipata msukumo wa kuchunguza viashiria vya kiujumi katika utanzu huu. Vijenzi vya kiujumi vilitumika ili kuweza kubainisha viashiria vya kiujumi katika riwaya teule za Kiswahili hususani za kimajaribio.

Utafiti huu ni wa maktabani na uwandani. Maktatabi utafiti huu ulifanyikia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo tulifanikiwa kuzifikia maktaba na makavazi zilizopo chuoni hapo. Maktaba Kuu ya Dkt. Wilbert Chagula na makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili zilitumika kusomea. Hivyo mkoa wa Dar es Salaam nchini Tanzania uliteuliwa ambapo mtafiti alisoma nyaraka mbalimbali na riwaya teule ili kupanua welewa juu ya masuala mbalimbali kuhusiana na makala haya. Sampuli ya vitabu teule vya riwaya yaani *Bina-Adamu!*[2] (2002) ya Kyallo Wamitila na *Dunia Yao*[3] (2006) ya Said Mohamed vilihakikiwa. Aidha, uwandani utafiti huu ulifanyika katika Majiji mawili ya Dar es Salaam na Nairobi. Jiji la Dar es Salaam liliteuliwa ili kuifikia sampuli lengwa ya wasomaji wanafunzi wa Shahada za Awali (SA)[4] na Shahada za Umahiri (SU)[5] katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Saalam waliteuliwa. Uteuzi wa sampuli hii unatokana na sababu kwamba wanafunzi hawa wamefikia viwango vya juu vya elimu na kwamba vitabu teule vya kimajaribio hutumika zaidi katika viwango hivyo ikilinganishwa na elimu ya msingi na sekondari[6]. Mtafiti aliwapa wasomaji wanafunzi riwaya hizo teule, walisoma kwa makini kwa muda wa mwezi mmoja kisha walitoa taarifa kwa njia ya insha[7] na mijadala ya vikundi[8]. Pia Jiji la Nairobi nchini

[2] Itajulikana kama R1

[3] Itajulikana kama R2

[4] SA walihusika kusoma riwaya zote mbili ambapo jumla walikuwa wanafunzi 120 waliogawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza la wanafunzi 60 nalo liligawanywa katika makundi 6 ambapo yalipatikana makundi ya SA1 hadi SA6. Kundi la pili pia lenye wanafunzi 60 liligawanywa kwa sita na kupata makundi sita yenye SA6 hadi SA12. SA1 hadi SA6 walisoma Riwaya ya *Bina-Adamu!* Na SA6 hadi SA12 walisoma riwaya ya *Dunia Yao*.

[5] SU walihusika kusoma riwaya zote mbili. SU walikuwa 8 hivyo waligawanywa katika makundi mawili ya wanafunzi wane kila kundi. SU1 walisoma riwaya ya *Bina-Adamu!*, na SU2 walisoma riwaya ya *Dunia Yao*.

[6]Tom Olali, usaili, 17/02/2020.

[7] Kwa wasomaji wanafunzi wa SA

[8] Kwa wasomaji wanafunzi wa SU

Kenya liliteuliwa ili kuifikia sampuli teule ya waandishi wa riwaya hizi, ambapo mtafiti alipata data kwa njia ya usaili.

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi. Hii ni nadharia iliyoanzishwa na Louise Rosenblatt mwaka 1978. Mwitiko wa Kiujumi kwa mujibu wa Rosenblatt (1985) ni mvuto anaokuwa nao msomaji katika matini na athari inayojitokeza kwa msomaji kutokana na maingiliano kati ya matini na msomaji. Ama kuhusu utokeaji wa mwitiko wa kiujumi Rosenblatt anaeleza kuwa,

> *"An aesthetic response occurs when the readers broaden their attention "to include the personal, affective aura and associations surrounding the words evoked and must focus on—experience, live through—the moods, scenes, situations being created during the transaction".* (Rosenblatt, 1985: xvii)

Mwitiko wa kiujumi hutokea "pale ambapo msomaji hupanua uzingativu wake katika kujihusisha yeye binafsi kwenye matini, kujiunganisha na mambo yanayomchoma moyo na kumwathiri kutokana na tajriba yake kwa maneno yanayovuta hisia na kumfanya ajiegemeze katika uzoefu wa maisha yake (tajriba), ushindi wa mambo aliyowahi kupitia, mandhari na hali ambayo hujengeka wakati wa maingiliano hayo. (tafsiri hii ni yetu).

Katika Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi matini na msomaji ni elementi mbili ambazo moja huitegemea elementi nyingine yaani elementi moja huwa na nafasi kubwa zaidi ya kiutendaji kuliko nyingine. Elementi hiyo ni matini yaani mawazo ya mwandishi (Crockett, 1998). Rosenblatt anaendelea kueleza kuwa, matini ndiyo inayomlazimisha na kumwongoza msomaji ili kupata mwitiko. Anadai kuwa;

> *"He will be conscious always that the words of the author are guiding him; he will have a sense of achieved communication, sometimes, indeed of communion withthe author. But it will be by virtue of the reader's own unique form of literarycreativity"* (Rosenblatt 1978, uk 50).
>
> "Atakuwa akijua wakati wote kwamba maneno ya mwandishi yanamwongoza; atakuwa na hisia za mawasiliano yaliyofanikiwa, wakati mwingine, mawasiliano ya moja kwa moja na mwandishi. Lakini itakuwa kwa sababu ya uwezo wa kipekee wa msomaji wa muundo wa ubunifu wa kifasihi. (tafsiri hii ni yetu)

Mawazo haya yanaungwa mkono na Wang (2011) anapoeleza kuwa, katika mchakato wa msomaji kujenga taswira, msomaji hawezi kuwa na uhuru wote wa kuiumba taswira hiyo kwa sababu hudhibitiwa kwa namna fulani na matini. Kimsingi nafasi ya msomaji haipo katika matini bali matini ndiyo humpa msomaji kazi ya kutenda. Wang anahitimisha kuwa, ikiwa matini inaeleza mawazo ya kuhuzunisha, msomaji atajenga taswira ya huzuni kisha kuhuzunika. Rosenblatt (1978) anasisitiza kuwa,

> "Or, we can say, the text produces a response in the reader--the text acts on the reader" (16)
>
> "Au, tunaweza kusema kuwa, matini huzalisha mwitiko kwa msomaji, matini hutenda ndani ya msomaji." (tafsiri hii ni yetu).

Douglas (1998) anaeleza kwamba, nadharia hii inaonesha uhai wa uhusiano kati ya msomaji na matini ambapo msomaji ni mtendaji anayejibu kwa kihisia za kimvuto kutoka katika matini. Matini hutumika kama kichocheo cha mwitiko wa mambo ambayo yanaweza kuwa ni mapya au yanamkumbusha aliyo na uzoefu nayo, kumfafanulia au kumchambulia zaidi ya vile alivyokuwa anayafahamu. Msomaji anaposoma matini anajikuta kurejelea kumbukumbu, mawazo au hisia za zamani alizo nazo au mpya anazozipata katika matini na kumwachia uzoefu mpya.

Kutokana na maelezo hapo juu tunaweza kuweka mawazo ya mwongozo kama ifuatavyo: Kwanza, msomaji huongozwa na mawazo ya mwandishi katika matini ili kupata mwitiko wa kiujumi. Pili, matini ndiyo mwegemeo mkuu wa mawazo ya kiujumi kwa maana kwamba hakuna mawazo ya ziada yanayotumika ili kupata au kujaliza mawazo ya mwandishi. Tatu, uhusiano wa kimawazo kati ya msomaji na kazi ya mwandishi ni pale msomaji anapohusisha sehemu tu ya uzoefu wake wa kiujumi kati ya mwingi aliyonao kutokana na mawazo yake kuongozwa na mawazo ya mwandishi wa kazi husika. Nne, matini huwa na nafasi kubwa zaidi na ndiyo inayozalisha miitiko kwa msomaji.

**Viashiria vya Kiujumi katika Riwaya Teule za Kiswahili**

Makala haya yamefanikiwa kubainisha viashiria vya kiujumi kwa kujikita katika vijenzi vitatu vya kiujumi ambavyo ni lugha, wahusika na usimulizi. Watafitiwa walisoma na kujibu swali lililowauliza, ni vijenzi gani vya kiujumi kati ya vilivyoorodheshwa (katika mwongozo wa swali) vimewavutia? Pia, mvuto huo umewaathiri vipi? Katika kujibu swali lenye vipengele hivyo viwili, wasomaji wanaonesha namna vijenzi vya kiujumi vilivyowavutia kisha athari walizozipata kutokana na mvuto walioupata. Viashiria vya kiujumi vilivyobainishwa vimejadiliwa kama ifuatavyo.

**Kijenzi cha Kiujumi cha Lugha**

Makala haya yamebaini kuwapo kwa kiashiria cha kiujumi cha lugha ya ukali katika kukemea utandawazi na athari zake katika nchi zinazoendelea. Imebainika kwamba waandishi wamewavutia wasomaji kutokana na ujasiri wa matumizi ya lugha ya ukali dhidi ya utandawazi na madhara yake kwa nchi za dunia ya tatu. Mvuto unaojitokeza hapa ni namna mwandishi alivyoubeba ujasiri wa kutumia lugha ya ukali tena kwa uwazi kukemea mataifa makubwa yaliyoendelea kiuchumi kuyanyonya mataifa madogo kiuchumi kwa kigezo cha utadawazi. Lugha hii imeamsha hisia za ujasiri na uthubutu dhidi ya woga na ujinga uliofumbatwa katika misingi ya kiutandawazi. Mwitiko wa hisia hizo unaonesha ufaafu wa Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi kwamba msomaji hupata hisia kutokana na namna mwandishi alivyoiwasilisha kazi yake ili kuamsha hisia kwa msomaji (Wang, 2011). Kutokana na mawazo haya ya kinadharia watoa taarifa[9] wanakiri kuwa mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* (2002) ni kama amevurugwa na mwenendo wa dunia ya sasa kwa sababu amejitoa mhanga kukemea kwa wazi tabia mbaya za mataifa makubwa yanayonyonya uchumi na rasilimali za mataifa madogo yanayoendelea kwa sababu ya utandawazi. Utandawazi umeharibu mifumo mingi kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia, jamii, taifa, bara na dunia kwa ujumla. Njogu (2006) anakiri kwamba, inatosha nikiwaambia kuwa ujasiri wa mwandishi umeimarika sana kwa kujadili mambo nyeti kuhusu jamii na mataifa ya Afrika kwa ujumla. Kwa mfano mwandishi katika riwaya ya *Dunia Yao* (2002) anasema:

> … Na lilipotimka lilitifua kila kitu dhaifu katika kasi na mikiki yake. Kila kitu kilipojaribu kufukuzana nalo, kilijikuta kinawachwa nyuma milioni ya kilomita. Likapita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likiripuka mandimi ya moto yaliyounguza na kukausha kila kitu: watu, wanyama, barabara, majumba, miji na majiji, mashamba, mazao ya chakula, mazao ya mauzo, miti, maji, hewa, pwani, bahari, nchi kavu, madini, umeme, mafuta, hospitali, madawa, benki, viwanda, biashara, rasilimali zote … shule, vyuo, desturi, mila, tamaduni na hata uhai, heshima na mustakabali wa watu-hata roho zao. Lilipenya hata ndani ya nyumba na vibanda vya watu kusasambura na kupekua kila kitu, kukashifu na kufedhehi na kisha kuangamiza lilivyopenda. Liliingia humo na kutawala na kuamrisha na kulazimisha mambo katika nyumba yake mwenyewe mtu (uk. 206).

Athari ya ujumi unaopatikana katika dondoo hili ni kuwazindua wasomaji juu ya madhara ya utandawazi ambayo hadi sasa hayana mipaka katika jamii zetu[10]. Vilevile watoa taarifa wakirejelea chanzo cha migororo katika familia, ndoa na watu katika jamii kwa ujumla wanaona inasababishwa na utandawazi hivyo mwandishi amejenga namna mpya ya kujenga uhusiano katika familia, ndoa na jamii kwa ujumla kutokana na mrengo hasi wa utandawazi dhidi ya mataifa madogo. Suala la upya linalodokezwa katika athari hii linaungana na mawazo ya kinadharia ambayo Douglas (1998) anadai kwamba matini ni kichocheo cha mwitiko wa mambo ambayo yanaweza kuwa ni mapya, au yanamkumbusha msomaji yale aliyo na uzoefu nayo, kumfafanulia au kumchambulia zaidi ya vile alivyokuwa anayafahamu. Uzoefu mpya unaoongezeka kwa msomaji kutokana na matini huonesha athari ya matini kwa msomaji.

[9] SU2

[10] SU2

Vilevile waandishi wanaeleza bila kificho athari za utandawazi kwa Mwafrika katika kumfanya tegemezi wa kila kitu kutoka mataifa makubwa kiuchumi na kiteknolojia kuanzia katika maisha ya mtu binafsi kama vile kufikiri, kuamua, kutibiwa, kusoma na kadhalika. Hali hii imeonekana kuondoa thamani ya Mwafrika kisha kuishia kuwatukuza Wamagharibi[11]. Kwa mfano msimulizi katika riwaya ya *Dunia Yao* anasema:

> Wamechukua kila kitu! Niliendelea. Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. Watendaji wetu. Wanaohisi kwa ajili yetu. Wanaona njaa na kiu zetu. Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kiujumla waendesha maisha yetu yote. Sehemu ya viwiliwili na akili zetu. Kwa ufupi wao ni kila kitu chetu! Sisi wengine ni mapipa matupu. Hatuna rojo la uhai. Hatuna supu ya maisha. Wala nyama ya ubinadamu. Hatuna sehemu ya utu. Hatuna rai. Hatuna maoni. Hatuna chetu. Hatuwezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi zetu (uk. 43)

Vilevile katika riwaya ya *Bina-Adamu!* (2002) msimulizi asema kuwa:

> Mimi ndiye ninayemiliki maisha yako. Nina uwezo wa kuchezea ninavyotaka bila hofu ya kudadisiwa na ye yote. Hii ni zamu yangu! Ndiwe chanzo cha dhiki wewe! Hapana! Umekosea. Mimi ndiye chanzo cha furaha ya kijiji. Vyakula vyote, ujuzi wote, elimu yote, tuseme raha zote na ndoto pia! (uk. 63)

Watoa taarifa wanakiri kuibua hisia za hasira, ghadhabu na hali ya kuukasirikia mfumo wa kisiasa ambao unaruhusu hali hii kuchukua nafasi katika nchi za Kiafrika. Athari ya ujumi huu ni kuwajengea wasomaji misingi mipya ya kujitathmini kuhusu maisha yao wenyewe dhidi ya mataifa makubwa[12]. Matokeo haya ya mwitiko wa kiujumi yanaungana na mawazo ya Wang (2011) kuwa matini huchochea hisia ambazo mwandishi hufanikiwa kuziibua kwa msomaji kwani kama matini inaeleza mawazo ya kuhuzunisha, msomaji atajenga taswira ya huzuni kisha kuhuzunika. Hivyo athari inayoelezwa na wasomaji hawa inaonesha kufanikiwa kwa nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi.

**Kijenzi cha Kiujumi cha Wahusika**

Wahusika ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi za fasihi (Njogu na Chimerah, 1999; Senkoro, 2011). Madumulla (2009) anawagawa wahusika wa fasihi katika aina mbili ambazo ni wahusika wakuu na wahusika wadogo au wasaidizi. Wamitila (2003:125) anaeleza kuwa wahusika wakuu hubeba kiini cha dhamira na maudhui ya kazi inayohusika pamoja na maana ya hadithi hiyo. Kutokana na mawazo haya, mhusika mkuu ameumbwa makusudi kutekeleza majukumu fulani anayodhamiria mwandishi. Matendo yake, furaha yake, machukizo yake na kuwepo kwake kunadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya mwandishi. Wamitilia (2002) anatambua kuwapo kwa aina hizi za wahusika lakini anatahadharisha kuwa kuna wahusika tuliowazoea katika baadhi ya kazi na wale ambao hatujawazoea. Anaendelea kueleza kuwa, kutokuwapo kwa wahusika wenye sifa za wahusika tuliowazoea ni sehemu ya uhusika kwenye riwaaya ya Kiswahili ya kimajaribio.

Katika makala haya kijenzi hiki kimeonekana kuwavutia na kuwaathiri wasomaji kutokana na namna waandishi walivyowatumia wahusika wasio binadamu wa kawaida. Wahusika wanaojitokeza katika riwaya hizi si wa mwili na roho[13] lakini matendo, tabia na mienendo waliyovikwa katika hadithi yamekuwa na mvuto mkubwa wa kuigwa, kushangaza na kuibua maswali mengi yanayochochea fikra kwa msomaji. Wahusika hawa hawana urazini wa binadamu wa kawaida. Hawa ni wahusika picha wanaozuka na kutoweka ghafla. Kutokana na hali hii tumebaini kuwapo kwa kiashiria cha kiujumi cha mshituko, taharuki, mashaka na woga ambacho kinaongeza hali ya kufikiri zaidi juu ya matukio yanayofanyika na kusababisha wasomaji kujiuliza maswali mengi juu ya

[11] MH4, hojaji 21/09/2021

[12] SA1

[13] Khamis (2007b)

matukio hayo kama vile kwa nini yanatokea, ili iweje, hatima yake ni nini? Kwa mfano, suala la kupigwa mateke, makofi na kupita katika mito ya ajabu, misitu ya kutisha na mapango makubwa kwa mhusika msimulizi binadamu katika riwaya ya *Bina-Adamu!*

Suala la wahusika kujitokeza kiajabuajabu linajitokeza pia katika riwaya ya *Dunia Yao*. Mwandishi wa riwaya hiyo anawatumia wahusika vivuli kuanzia msimulizi na wahusika wengine (uk. 3, 4, 8, 27, 28 n.k.). Kwa mfano msimulizi anaeleza:

> Aliyeinuka sasa katika lile albamu alikuwa Bi M aliingia ndani ya hisia zangu na kunikera nimtie katika simulizi yangu. Jazba ikanipanda. Ile jazba ya kiandishi (uk. 18) … Ghafla nilimwona Bi M akinyanyuka penye albamu nililokuwa nikilitazama (uk. 20). Sasa aliinuka Yungi katika lile albamu. Bi M akawa kasimama vilevile. Hakwenda kulala kwenye bapa katika albamu (uk. 23).

Watoa taarifa wanakiri kwamba taharuki ikizoeleka na msomaji anapoendelea kusoma hufikia kuyaona maajabu hayo kuwa ya kawaida kwa kuwa tu msomaji anakuwa amejengwa au kupata tabia ya ujasiri wa kuyaona matukio haya ya ajabu yanawezekana. Athari ya pili ni kuongeza uwezo wa kufikiri juu ya uwezekano wa maisha ya kiajabu katika maisha halisi[14]. Watafitiwa wanaeleza namna masuala hayo yanavyoweza kudhihirika katika maisha halisi na kwamba ni mara nyingi mambo yanayodhaniwa kuwa hayawezekanai huwa yanawezakana na baadaye kuwa ya kawaida.

Kutokana na matumizi ya wahusika vivuli tena wanaotokea katika albamu lililopo ukutani, wasomaji wanaona si jambo la kawaida lakini lina maana gani? Mvuto wao unaelekea kumwelewa mwandishi kwa namna anavyoona kuvuliwa kwa thamani, heshima na utu wake pamoja na watu wa jamii yake katika riwaya ya *Dunia Yao* na kutawaliwa na mwenendo wa maisha ya dunia ya wengine kiasi kwamba wao wanaonekana si watu tena bali vivuli tu[15]. Ujumi huo unathibitishwa na msimulizi kwa kusema:

> Kila mtu anadhani mimi chakaramu, kama si mwendawazimu kamili! Hali ya mwendawazimu si mwendawazimu, timamu si timamu, ingawa ni bora kuliko watu wengine! Unafanyaje unapokosa kuzungumza na mtu mwingine ila nafsi yako mwenyewe tu? Lazima niseme na kivuli changu na kivuli changu kiseme na vivuli vingine. Viumbe pekee vilivyobaki kuzungumza navyo na kuvielewa kama vinavyonielewa. Viumbe ninavyoviweka kichwani na kisha kuvisimamisha karatasini! Nahisi lazima nizungumze navyo kama nataka kubaki. Kubaki si kuishi tena" (uk. 3). "Mwisho, (na muhimu zaidi), limebaki rojo tupu la bongo; rojo la kuchambulia mambo. La kuumbia na kuumbua vivuli vya watu. La kutolea dukuduku la moyo katika sanaa ya aina hii (uk. 4). Nikajifunza kompyuta kwa bidi kwani nilijua ni mwokozi wangu katika maisha ya upweke na unyamavu. Ya kusema kimyakimya na vivuli vya nafsi yangu- yaani wahusika wangu. (uk. 8).

Athari ya kiashiria hiki kwa wasomaji ni kuchochea hasira ya kupambana ili kurudisha heshima, thamani na hadhi ya mtu mweusi katika dunia yake[16]. Athari hii inaonekana kumkumbusha msomaji juu ya asili yake. Kutokana na kiashiria na athari hii ya kiujumi tunaona kuwa msomaji ameweza kukumbuka asili yake, moja ya wazo muhimu katika nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi kwamba msomaji huweza kupata athari na kumjengea tabia njema kwa kumkumbusha, kumwongezea au kumpatia taarifa mpya (Wang, 2011).

Mbali na athari hizo utafiti huu unaona kwamba riwaya hizi kwa kiasi kikubwa zinawaathiri wasomaji katika kutafakari, kufikiri na kujipambanua kutokana na namna wahusika wanavyobeba uhusika na matukio wanayokumbana nayo. Hali hii inaonekana pale wahusika wanapobeba jukumu kubwa na zito ambalo ili lifanikiwe mhusika mkuu anakumbana na masaibu mengi ya ajabauajabu.

[14] SA4

[15] SU2 mijadala ya vikundi, 29/09/2020, na SU3 mijadala ya vikundi, 30/09/2020.

[16] SA12, SA13 na SU3 mijadala ya vikundi, 30/09/2020

Kwa mfano mtoa taarifa[17] anaeleza namna mhusika mkuu katika riwaya ya *Bina-Adamu!* anavyosababisha msomaji ajiulize maswali kadha wa kadha huku yakikosa majibu:

> Msomaji anajikaza kujua nini hasa kinachomchochea mwandishi kuwachora wahusika kama anavyowasawiri? Ana malengo yapi? Yaani swali 'kwa nini?' ndilo linaloongoza usomaji na kuvuta umakini wa msomaji vinginevyo huenda asielewe kinachosimuliwa. Kuanzia mwanzo wa riwaya tunajiuliza huyu mhusika nguli au shujaa anayefunga safari kuelekea kitovu cha kijiji chao ambacho kinaogopwa ana kusudi gani? Kwa nini awe mkaidi kiasi hicho? Anapoaza kukabiliana na changamoto kwenye safari yake tunajiuliza, nini maana ya changamoto hizo? Kupigwa makofi na mateke kuna maana gani? Kuongozwa na mizimu isiyoonekana bali inasikika tu ina maana gani? Kupewa fimbo ya kumkokongoja kuna maana gani? Kupewa kibuyu chenye rojo kuna maana gani? Kucharazwa viboko kuna maana gani? Kuanguka kwenye mto unaosafiri kwa kasi na maji yake yanarudi nyuma kuna maana gani? Mvuto umo kwenye kusaka majibu ya maswali haya yanayomtatiza msomaji kutokana na usawiri wa wahusika usiokuwa wa kawaida. Changamoto hii ya kukwea mlima wa masimulizi hadi kileleni ndiyo inayomvuta msomaji mvuto wa riwaya hii yenye ugumu.

Dondoo hili linadhihirisha namna mwandishi anavyoiteka akili ya msomaji na kujikuta badala ya msomaji kuielewa matini, hujikuta amejiegemeza katika kutaka kuielewa akili ya mwandishi ina maana gani. Maelezo ya mtoa taarifa huyu yanaonesha namna nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi inavyodhihirika kwani tunaona msomaji alivyojizamisha yeye binafsi katika kutaka kuilelewa akili ya mwandishi huku akijirudia uzoefu wake wa kiujumi. Hapa ndipo Rosenblatt (1985) anapoeleza kuwa msomaji hupanua uzingativu katika kujihusisha yeye binafsi kwenye matini, kujiunganisha na mambo yanayomchoma moyo na kumwathiri kutokana na tajriba yake kwa maneno yanayovuta hisia na kumfanya ajiegemeze katika matini kadiri ya uzoefu wa maisha yake. Kwa kutumia kijenzi cha wahusika wasomaji wamejikuta kujizamisha katika mawazo ya kina ya mwandishi.

**Kijenzi cha Kiujumi cha Usimulizi**

Kimsingi, hadithi haiwezi kumfikia msomaji bila kuwapo usimulizi wa hadithi yenyewe. Usimulizi upo wa aina nyingi kama vile, usimulizi anuwai, ngazi, maizi, penyezi au dukizi, sawia, tangulizi, wa kiutendi, wa kiurejeshi, wa kiutomaji, usimulizi wa nafsi ya kwanza, wa nafsi ya pili na ule wa nafsi ya tatu (Wamitila, 2003:325-327 na 2006:41). Wamitila (2003) anaeleza kuwa, usimulizi wa nafsi ya kwanza ni usimulizi wa hadithi unaofanywa na mhusika kwa nafsi ya kwanza. Mhusika huyo anaweza kuwa mshiriki wa matukio au matendo ya hadithi au asiwe mshiriki. Usimulizi huu hujenga uhusiano wa karibu kati ya hadithi na msomaji. Kutokana na data za utafiti huu, aina hii ya usimulizi ndiyo inayojitokeza kwa kiasi kikuwa katika riwaya hizi teule kiasi cha kuwavutia na kuwaathiri wasomaji kwa kiasi kikubwa katika namna tofautitofauti.

Kijenzi cha kiujumi cha usimulizi kimewavutia wasomaji kwa namna mbalimbali. Makala haya yamebaini usimulizi wa nafsi ya kwanza ulivyochochea hisia za msomaji kujihisi mhusika wa hadithi. Usimulizi umewaingiza wasomaji katika hadithi kwa hisia kali na kuwazamisha kiasi kwamba wanahisi wanachokihisi wahusika, wanahusika na matukio, visa na kila kitu katika hadithi kupitia msimulizi[18]. Mwitiko huu unabainika kutokana na madai ya Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi kuwa, msomaji hujikuta anamakinika na kujiegemeza katika matini na kujikuta ni sehemu ya matini (Clark, 1970). Kwa mfano, katika riwaya ya *Bina-Adamu!* wasomaji huanza kujiingiza katika hadithi msimulizi anapoanza kusimulia kuhusu matatizo ya kijiji[19]. Kiashiria cha kiujumi kinachoibuliwa hapo ni ile hali ya kujihisi mhusika anayeyaishi matatizo ya kijijini na anayepata ufahamu kuwa kuna chanzo cha matatizo hayo. Lakini wanakijiji wengi wameshindwa kuyatatua kwa sababu ya vikwazo vilivyopo katika kujihusisha na matatizo hayo. na maamuzi yake ya kutaka kuyashughulikia (uk. 1-

[17] MH2, hojaji, 17/04/2021

[18] SA1, SA3, SA4, SA5, SA6; SA7, SA8, SA10 na SA12

[19] Wansomaji wanafunzi wa SA karibu wote waliosoma riwaya hii wanakiri kujiona ndiyo wahusika wa hadithi ya riwaya hii ktutokana na namna usimulizi wa nafsi ya kwanza ulivyotumika.

13). Viashiria hivi vinajitokeza kutokana na wasomaji kujiuliza baadhi ya maswali kama vile, hiki ni kijiji gani? Kwa nini kina mambo mengi ya ajabu kiasi hiki?[20] Kutokana na kiashiria hiki wasomaji walionesha kupata athari ya kujenga tabia ya kuthamini matatizo ya jamii na kuwa na maamuzi ya kuyashughulikia.

Kiashiria kingine cha kiujumi kinachojitokeza katika riwaya ya *Bina-Adamu!* ni maamuzi ya kuanza safari ili kutafuta kiini cha matatizo ya kijijini. Kiashiria hiki kinatokana na mvuto unaotokana na msimulizi kuchukua hatua ya kuanza safari kutafuta uvumbuzi wa matatizo ya kijiji, kumebainika kuchochea hisia na ari ya utayari wa kuanza kukabiliana na matatizo yanayoikumba jamii yake inayomzunguka[21]. Msimulizi anathibitisha kwa kueleza kuwa:

> "Nilikuwa bado nimesimama niliposhtukia nimepigwa teke la nyuma na kuambiwa, "haya anza safari yako ya uvumbuzi, unangojea nini?" Nilitii. Huko mbele niliweza kuona viunzi kadha vya binadamu (vilikuwa mifupa tupu iliyotoa mwangaza). Niliamua kuvifuata. Nilipokuwa nikipita kufuata viunzi hivyo nilisikia sauti ya kila aina. "Jifunikeni shuka anakuja, huyu. Je, ataweza lakini? Nilitamani kuwaambia nitaweza ingawa sikujua kilichokuwa kikitajwa na sauti hizo" (uk. 12).

Mvuto unaotokana na msimulizi katika usimulizi wa nafsi ya kwanza umewafanya wasomaji kujua umoja, ushirikiano, mshikamano wa jamii nzima ndiyo ushindi wa jamii dhidi ya chanzo cha matatizo katika jamii. Data zinaonesha kuwa wasomaji wanapata furaha, ridhiko, amani na faraja inayopatikana baada ya kuujua ukweli na mbinu zinazoweza kuwasaidia kupambana na matatizo ya kijijini. Kwa kutumia msimulizi watoa taarifa[22] wanaonesha hali hii pale msimulizi anapotoa suluhu ya matatizo ya kijiji kuwa:

> "Jamii inahitaji kujielimisha upya kuanzia chini hadi juu, mtoto hadi mzee, wote.. e.e. huu ndiyo ukombozi ufaao; matakwa ya jamii yawekwe mbele. Kumbuka siku za ukombozi kuletwa na mtu mmoja" (uk. 154). "Unganeni kiuchumi, kisiasa na kijamii. Umoja ni nguvu! Mtaishia kumfunga ye yote japo awe mkubwa" (uk. 155).

Kiashiria hiki kinaleta athari kwa msomaji kuzidi kupambana bila kujali hali yoyote katika mazingira yoyote ya kuutafuta ukweli kwani hatima ya magumu ni mafanikio[23]. Pia athari nyingine ni kumjengea msomaji tabia ya kuujenga umoja na mshikamano wa jamii nzima hidi ya changamoto zinazoikumba jamii[24]. Kwa ujumla viashiria vya kiujumi vimeonekana kuacha athari chanya kwa wasomaji kwani wasomaji wanaonekana kujiingiza moja kwa moja kihisia na hivyo kutoa mitazamo, misimamo na baadhi ya shauku za kuanza kushughulikia yale waliyoona ni matatizo yanayopaswa kushughulikiwa.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza umejitokeza pia katika riwaya *Dunia Yao*. Tofauti na ule wa riwaya ya *Bina-Adamu!,* data zinaonesha kwamba usimulizi unaojitokeza katika riwaya hii ni kuwapo kwa msimulizi ambaye pia ni msimuliwaji. Hali hiyo imeipa kazi hii mwonjo wa kitawasifu[25] (uk. 2). Mvuto unaojitokeza katika riwaya hizi kiasi cha kuibua viashiria vya kiujumi ni ule ubingwa wa mwandishi kuichora picha ya jumla ya dunia ya leo na kwamba amewahi sana kuonesha matatizo yake mengi kwa jinsi ya kuvutia kutokana na sanaa yake; mambo hayo yanaeleweka zaidi hivi leo[26]. Anatolea mifano baadhi ya mambo hayo kuwa ni athari ya utandawazi na hali halisi ya unyonyaji wa mataifa yaliyoendelea katika mataifa changa. Athari inayoonekana hapa mtoa taarifa huyo anadai

---

[20] Kijiji kinachomaanishwa hapa ni dunia (dunia kama kijiji), na kiini cha kijiji ni Marekani. Ufafanuzi huu unatokana na mwandishi wa kitabu hiki kwanza katika blabu, pili katika hadithi yake, (*Bina-Adamu*!: 86)

[21] SA1, SA5

[22] SA4

[23] SA1, SA4 na SA5,

[24] SA1, SA3, SA5 na SA6.

[25] SA8, Waliaula (2010:147-148)

[26] MH4 hojaji 21/09/2021

kwamba ipo haja ya kupambana dhidi ya mataifa makubwa yanayotumia utandawazi kama silaha yao ili kuyaruhusu mataifa machanga kukua kiuchumi na kiutamaduni.

Usimulizi wa kitawasifu unaibua kiashiria cha kiujumi cha kujihusisha katika sanaa. Msomaji anajikuta kujipiga picha kutokea katika hadithi na kwamba kuisoma hadithi hii ni kama anajisoma mwenyewe[27]. Kwa mfano msimulizi kujiona yupo lakini hayupo; kajivuruga (uk. 1), kujitia uwendawazimu lakini wenye utimamu (uk. 8), kueleza historia yake kama shule, vyuo na kazi alizofanya (sura ya pili), baadaye anapata ugonjwa wa ajabu, hapo ndipo anachanganya ubunifu na baadhi ya taarifa ambazo ni kama za kweli lakini katika hali ya kiubunifu. Jambo la kuvutia zaidi ni namna anavyofanya hadithi hii kuwa ya wananchi wote[28]. Msimulizi anaeleza kwamba:

> "Ndi- akamweleza binti yake hadithi yake mwenyewe Ndi-. Na hadithi ya Ndi- sasa si hadithi yake mwenyewe tu, bali ya jirani yake, na pia ya wananchi wake. Kwa kweli ni hadithi ya nchi yake. Hadithi mpya na kongwe … Na kwa kweli hiyo ya kusimulia hadithi hii muhimu Ndi- alijizuia kufa. Kwa kuing'ang'ania sanaa mpya. Sanaa ya usimulizi ya mdomo na maandishi. Sanaa mpya. Sanaa ya miujiza inayoelezea miujiza ya jamii" (uk. 211).

Athari ya kiashiria hiki ni kumjengea msomaji tabia ya kuwa na hamu, shauku na ari ya kuyaona matatizo ya jamii ya leo kwa namna ya uangalifu sana. Tabia ambazo ni matokeo ya mawazo ya mwandishi ambapo kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Kiujumi matini huzalisha hisia kali zinazomjengea msomaji tabia kutokana na namna mwandishi anavyowasilisha mawazo yake (Wang, 2011).

Mjadala wa makala haya umebaini viashiria vya kiujumi mbalimbali kutoka katika riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio kwa kutumia vijenzi vitatu vya kiujumi ambavyo ni lugha, wahusika, na usimulizi. Data kutoka kwa watoa taarifa wasomaji wanafunzi na waandishi wamethibitisha kuwapo kwa viashiria vya kiujumi katika riwaya teule za *Bina-Adamu!* (2002) ya Wamitila na *Dunia Yao* (2006) ya Mohamed. Hivyo kutokana na mjadala huu makala yamethibitisha kuwapo kwa ujumi katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio na maendeleo ya jamii ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Kutokana na viashiria vya kiujumi ni wazi kuwa riwaya hizi zina dhima za kiujumi. Dhima ambazo zinamjengea tabia mbalimbali msomaji katika kuyafikia matatizo yake kwani kwa kiasi kikubwa athari zilizojitokeza zinalenga kumsaidia msomaji katika mustakabali wa maendeleo ya maisha yake katika jamii pana ya Afrika Mashariki.

**Hitimisho**

Makala haya yamebainisha viashiria vya kiujumi kwa kutumia data kutoka kwa watoa taarifa wanafunzi na waandishi. Kutokana na mjadala katika makala haya ni wazi kuwa, suala la riwaya za kimajaribio kuwa na ujumi si suala linalohitaji kuwa na mtanziko wa kuwapo kwake. Jambo la msingi ni ule uwezo wa kuelewa kile kilichoandikwa katika riwaya hizo. Makala yameona kuwa katika viashiria vingi vya kiujumi, kama asemavyo Mulokozi (20017) kuhusu dhima ya ujumi riwaya hizi zimeegemea katika kufikirisha, kutia moyo, kuukasirikia uovu wa mataifa makubwa dhidi ya mataifa machanga miongoni mwa dhima nyingine. Dhima hizi zinamtaka msomaji kujitafakari upya kwa mtazamo chanya. Hivyo, kutokana na mjadala wa makala haya ni wazi kuwa riwaya za mkondo wa kimajaribio zina ujumi kama ulivyobainishwa na kujadiliwa.

**Marejeleo**


Attard, J. (2018). The Connection between Literature and Aesthetic: Is it Problematic? in Symposia Melitensia. Number 14. https://www.um.edu.mt/library/oar/bitstream/123456789/30002/1/6.%20The%20Connection%20between.pdf: tarehe 17:2:2021 saa 15:48.

Armstrong, W. H. (Mh) (1879). *Aesthetics*. London: Bradburg, Agrew & Co. Printers.


[27] SU2, mijadala ya vikundi, 29/09/2021

[28] MH4 hojaji 21/09/2021

Barrett, M. S. (2002). Towards a ' situated ' view of the aesthetic in music education. *Journal of Aesthetic Education.* 36 (3 ), 67- 77.

Barrett, M.S. (2012). "Aesthetic Response" katika *The Child as Musician: A Handbook of Musical Development.* McPherson, G.E. (ed.) Newyork: Oxford University Press. 173-191.

Clark, W. H. (1970). "Literature as Exploration by Louise M. Rosenblatt" The Journal of Aesthetic Education, Apr., 1970, Vol. 4, No. 2, Special Issue: Curriculum and Aesthetic Education, pp. 150-153. URL: https://www.jstor.org/stable/3331557. tarehe 08/11/2021 saa 04:20 asubuhi

Douglas, W. (1979). "The Reader, the Text, the Poem. The Transactional Theory of the Literary Work by Louise M. Rosenblatt" CEA Critic, The Johns Hopkins University Press Vol. 41, No. 4, pp. 34-38. URL: https://www.jstor.org/stable/44378139. tarehe 08/11/2021 saa 04:20 asubuhi

Ferrari, G. R. F. (1999). "Aristostle's Literary Aesthetics" in *Phronesis*, Vol. 44. No. 3: 181-198

Gromov, M. D. (2004). "Post-modernistic Elements in Recent Kiswahili Novels," in *The Nairobi Journal of Literature*: The Journal of the Department of Literature, University of Nairobi, 2: 28-36.

Gromov, M. (2014). "Visions of the future in the 'new' Swahili novel: Hope in desperation?" Tydskrif vir letterkunde 51 (2): 40-51.

Gromov, M. (2016). "Local achievement' or 'external influence'? Intertextuality and political satire in the 'new' Swahili novel in Kenya". In Dunia Yao: Utopia/Dystopia in Swahili Fiction, edited by C. Vierke and K. Greven, 57-72. Koln: Rudiger Koppe.

Gromov, M. (2019). "Riwaya mpya", majina mapya, changamoto mpya: kuhusu maendeleo ya "riwaya ya majaribio" katika fasihi ya Kenya katika Eastern African Literary and Cultural Studies vol.5 NOS. 3-4 pp 200-213. URL. https://doi.org/10.1080/23277408.2018.1486497 tarehe. 01/03/2022 saa 3 asubuhi.

Henry, G. (2020). Uchambuzi Linganishi wa Ujumi wa Kifasihi katika Simulizi Teule za Watumwa kutoka Afrika, Amerika na Ulaya. Tasnifu ya PhD (Kiswahili). (haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jones, G. (1994). "From the Quest for Wholeness: Re-Imagining the African-American Novel: An Essay on Third World Aesthetics" in Callaloo, Spring, by The Johns Hopkins University Press. Vol. 17, No. 2 (Spring, 1994), pp. 507-518.

Kant, I. (1790), *Critique of the Power of Judgment*, Iliyotafsiriwa P. Guyer, na E. Matthews (2000), Cambridge University Press, Cambridge.

Khamis, S. A. M. (2007a). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili" katika *Kioo cha Lugha* Juz.5 F.EM.K. Senkoro na K.K. Kahigi (Wah). Dar es Salaam: TUKI: 11-23.

Khamis, S. A. M. (2007a). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili" katika *Kioo cha Lugha* Juz.5 F.EM.K. Senkoro na K.K. Kahigi (Wah). Dar es Salaam: TUKI: 11-23.

Khamis, S. A. M. (2007b). "Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai" katika *Kiswahili* juzuu.70. TUKI. Massamba, D.P.B. (Mh):47-66.

Kivy, P. (2011). *Once-Told Tales: An Essay in Literary Aesthetics*. Malden: Wiley-Blackwell Publication.

Lankford, E. L. (1992). *Aesthetics, issues, and inquiry.* Reston, VA: NAEA.

Lindi, L. M. (2012). "Ufasihi Simulizi katika Riwaya ya Kisasa ya Kiswahili: Mifano kutoka Nagona (1990) na Mzingile (1991)." Tasnifu ya M.A Kiswahili (Hijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Locke, J. (1975). *An Essay Concerning Human Understanding*. P.H.Nidditch (mh). Oxford: Cladendon Press.

Mbatiah, M. (1998). Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: Nagona na Mzingile katika Mulika 24, TUKI. Tumbo-Masabo Z.N.Z na Mdee J.S. (Wah) Chuo Kikuu cha Dae es Saalaam:1-11.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Kautu Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, C. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Pickens, T. A. (2014). "Octavia Butler and the Aesthetics of the Novel" Wiley Online Library, https://doi.org.10.111/hypa.12129. Tarehe 08/11/2021 saa 04:28 asubuhi.

Puolakka, K. (2019). "Structure Disclosed. Replete Moments and Aesthetic Experience in Reading Novels", International Journal of Philosophical Studies, 27:4, 544-561, DOI:10.1080/09672559.2019.1632371. https://doi.org/10.1080/09672559.2019.1632371. Tarehe 05/11/2021 saa 07:22 mchana

Rosenblatt, L. M. (1978). *The reader, the text, and the poem: The transactional theory of the literary work.* Carbondale, IL: Southern Illinois University Press.

Rosenblatt, L. M. (1985). The transactional theory of the literary work: Implications for research. In C. R. Cooper (Ed.), Researching response to liter- ature and the teaching of literature (pp. 33-53). Norwood, NJ: Able

Senkoro, F. E. M. K. (1983). Riwaya ya Kiswahili. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. M. E. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Walton, L. K. (1999). "Projectivism, Empathy, and Musical Tension', in The Philosophy of Sydney Shoemaker. Philosophical Topics: 26.No. 1/2 by University of Arkansas Press p.p 407-440. URL:http://www.jstor/stable/43154293. Tarehe 21/03/2021 saa 02:32 jioni.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publihers Limited.

Wamitila, K. W (2002). *Bina-Adamu!* Phoenix Publishers, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wang, D. (2011). "Iser's Theory of Aesthetic Response: Strategies on Compensation for Cultural Default in Translation, Perspectives, 19:4, 339-352, DOI: 10.1080/0907676X.2011.570352 https://doi.org/10.1080/0907676X.2011.570352. Tarehe 08/11/2021 saa 04:40 asubuhi.